


TANZANIA NATIONAL ROADS AGENCY



P.O Box 11364
3rd Floor
Maktaba Complex
Bibi Tili Mohamed Road
Dar es Salaam

Tarehe 20/11/2007

Kumbukumbu TRD/D/GEN/P.43/VOL.II/


Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
(Uwaba)
SLP 12247
Dar es Salaam.

YAH: TAARIFA KUHUSU USANIFU WA BARABARA ZINAZOJENGWA KATIKA JIJI LA
DAR ES SALAAM

SOMO: Taarifa za Barabara Zinazojengwa na Zinazopangwa Kujengwa

Tafadhalii rejea barua yako ya tarehe 8 October 2007 kuhusiana na somo tajwa hapo juu ikitutaka
kutoa ufanuzi zaidi wa maswali yaliyojibwa kwenye barua yetu kumbukumbu
namba TRD/D/GEN/P.43/VOL.II/ ya tarehe 10 Septemba 2007.

Kwa barua hii ninakutumia ufanuzi kwa maswali yako .


Wako katika ujenzi wa Taifa.

Ephraem C M Mrema
MTENDAJI MKUU

Majibu ya wapanda baiskeli UWABA.

1. Swali

Kwenye jibu la swali namba moja, barua yako inasema kwamba guta ni chombo cha ingine.Kwa sisi jina la guta lina maana ya baisikeli ya gurudumu tatu siyo chombo cha ingine. Basi, maguta yataruhusiwa kutumia njia ya baisikeli?

Jibu

Kwa madhumuni ya mradi huu guta limechukuliwa kama chombo cha moto. Hivyo maguta yote yatatumia njia za magari.

2. Swali

Kwa nini design ya barabara ya Nelson Mandela haina sehemu maalumu ya watembea kwa miguu ambayo ni tofauti na njia ya baisikeli.

Jibu

Barabara ya Mandela ni maalumu kwa ajili ya magari mazito yanayotoka na kuingia bandari ya Dar es Salaam.Barabara hii haikutarajiwa kuzungukwa na makazi ya watu na hivyo hapakuwepo na haja ya kuwekwa njia ya waenda kwa miguu.

Makazi yaliyo sambamba na barabara hii ni holela ambayo yamejengwa bila kuzingatia matumizi muafaka ya ardhi kulingana na maendeleo ya miji.Hata hivyo swala hilli tunaliangalia upya ili kupata uwezekano wa kuweka njia ya waenda kwa miguu.

3. Swali

Kwenye jibu la swali namba nne,barua yako inasema services roads zitakuwepo- hizi service roads ni sawa na njia za baisikeli au ni tofauti ? Magari yataruhusiwa kupita njia ya baisikeli au hapana?

Jibu

Service roads si sawa na njia za baisikeli. Aidha magari hayataruhusiwa kupita njia ya baisikeli.

4. Swali

Kutakuwa na ninii cha kuzuia magari kuingia njia za baisikeli? Kerbstones zitalinda sehemu ya baisikeli au sehemu za watembea kwa miguu tu? Kutakuwa na ninii kati ya njia ya baisikeli na njia ya magari?

Jibu

Magari hayawezi kuingia sehemu ya watembea,kwa miguui kwani kingo zilizojengwa sambamba na barabara haziwezi kuruhusu magari kuingia kwenye njia ya watembea kwa miguu. Kwa hiyo 'Kerbstones' zinazuia na kulinda sehemu zote za watu wanaofembea na baisikeli pamoja na watembea kwa miguu. Kama tulivyojibu hapo juu kutakuwa na vizuizi nya kuzuia magari na baisikeli yaani 'kerbstones'.

Michoro ya barabara ya Kilwa inaanisha majibu yetu vizuri tuliyoyatoa. Hakuna michoro iliyobadilishwa hata kidogo. Ujenzi wa barabara ya Sam Nujoma bado unaendelea na sehemu zote zilizowekwa kwenye michoro zitajengwa kama ilivyoonyeshwa.